

# CHUO CHA SERIKALI ZA MITAA



---

S.L.P. 1125, DODOMA Simu: 026- 2961101 Fax: 026 -2961100,  
Barua Pepe: [info@lgti.ac.tz](mailto:info@lgti.ac.tz)

Mkuu wa Chuo cha Serikali za Mitaa (Hombolo) anakaribisha maombi ya kujiunga na masomo kwa mwaka 2018/2019 katika ngazi ya Astashahada (Certificate) na Stashahada (Diploma) kwenye fani zifuatazo:-

1. Utawala katika Serikali za Mitaa (Local Government Administration)
2. Usimamizi wa Rasilimali Watu (Human Resource Management)
3. Maendeleo ya Jamii (Community Development)
4. Uhasibu na Fedha katika Serikali za Mitaa (Local Government Accounting and Finance)
5. Utunzaji wa Kumbukumbu (Records, Archives and Information Management)
6. Ununuzi na Ugavi (Procurement and Supplies Management)

## NAMNA YA KUOMBA KUJIUNGA NA MASOMO

1. Astashahada (NTA Level 4 - Basic Technician Certificate)

**Sifa:** Mwombaji awe amepata angalau ufaulu wa "D" 4 za Kidato cha Nne(CSEE). Masomo ya Dini hayahusiki.

2. Astashahada (NTA Level 5-Technician Certificate)

**Sifa:** Mwombaji awe amepata angalau ufaulu wa "Principal Pass" moja na "Subsidiary" katika mthani wa Kidato cha Sita (ACSEE) AU awe na Astashahada (NTA Level 4 Basic Technician Certificate) toka Chuo chochote kilichosajiliwa na kinachombulika na Serikali. Pia awe amepata angalau ufaulu wa "D" 4 za Kidato cha Nne(CSEE). Masomo ya Dini hayahusiki.

3. Stashahada (NTA Level 6 -Diploma).

**Sifa:** Mwombaji awe na Astashahada (NTA Level 5-Technician Certificate) toka Chuo chochote kilichosajiliwa na kutambuliwa na Serikali.

## ANGALIZO:

- i. Kozi ya Uhasibu na Fedha katika Serikali za Mitaa (Local Government Accounting and Finance) inahitaji mwombaji awe amefaulu somo la HISABATI katika mthani wake wa kidato cha nne.
- ii. Kama mwombaji amefanya mthani wa kidato cha nne zaidi ya mara moja, aambatanishe nakala za vyeti vyake vya awamu zote za mthani aliyofanya.

iii. Gharama za masomo na mchanganuo wa ada unapatikana katika ukurasa wa tatu(3) wa fomu ya maombi.

Fomu zinapatikana:

1. Chuoni, Hombolo
2. Kampasi ya Dodoma Mjini (Area C)
3. Katika tovuti ya Chuo [www.lgti.ac.tz](http://www.lgti.ac.tz)
4. Wizarani Ofisi ya Rais-TAMISEMI (Library)

Fomu iliyokwisha jazwa iambatanishwe na malipo ya ada ya maombi ya shilingi 10,000/=kwenye Akaunti Na. 50501100209 NMB. Jina la akaunti ni CHUO CHA SERIKALI ZA MITAA

Maombi yatumwe kwa mkono au kwa posta kwenda kwenye anuani ifuatayo:

**Mkuu wa Chuo,**  
Chuo cha Serikali za Mitaa,  
S. L. P 1125, **Dodoma.**

**MWISHO** wa kupokea maombi ni tarehe 31/05/2018

Kwa maelezo zaidi piga simu namba **0717 487 420/0754 415 659, 0755 241 010**